



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA

**MAAMUZI YA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI KUHUSU
RUFAA NANE (8) ZA WAGOMBEA UDIWANI KWA AJILI YA
UCHAGUZI MDOGO WA TAREHE 16 SEPTEMBER, 2018**

Kwa kuzingatia kifungu cha 44(5) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, kikisomwa pamoja na kanuni ya 28(1) ya Kanuni za Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2015, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilipokea Rufaa Nane (8) kutoka kwa Wagombea Udiwani wa Kata za Sisimba, Maanga, Nsalaga na Iwambi katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya; Kata ya Nkuyu katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela; Kata ya Kizota katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma na Kata ya Mwanhuji katika Halmashauri ya Wilaya ya Meatu.

Kwa kuzingatia matakwa ya kanuni ya 29(3), (4) na (5) ya Kanuni za Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2015, Tume, ilipokea, ilijadili na kufanya maamuzi ya Rufaa hizo Nane (8) ambazo kati ya hizo Rufaa, mbili (2) zilipinga kuondolewa kugombea na kutaka kurejeshwa kugombea na Rufaa sita (6) zilikuwa zikipinga wagombea walioteuliwa.

Tume imeamua kuwa wagombea saba (7) wataendelea na uchaguzi na Mgombea Mmoja ameenguliwa na hivyo kutoendelea kuwa mgombea.

Taarifa za maamuzi ya rufaa hizo, zimetumwa kwa wahusika kupitia kwa Wasimamizi wa uchaguzi wa Halmashauri husika.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inavikumbusha Vyama vya Siasa na Wagombea wao kuwa vinapaswa kuzingatia Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2015, wakati wote wa kampeni na hata Siku ya Uchaguzi.

Taarifa zaidi kuhusu maamuzi ya Rufaa hizo imeambatanishwa.

Imetolewa leo tarehe 30 Agosti, 2018 na:

Dkt. Athumani J. Kihamia
MKURUGENZI WA UCHAGUZI